



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA MERU



Unapojibu tafadhalii taja:

Kumb.Na.S.20/86/Vol.II/11

06.01.2022

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru anapenda kuwatangazia Watanzania wote wenye sifa kuomba nafasi ya Ajira za Watendaji wa Vijiji na Msaidizi wa Kumbukumbu kwa masharti ya kudumu. Tangazo hili ni baada ya kupokea vibali vyatia ajira mbadala vyenye Kumb.Na. FA.170/371/O1"A"/121 cha tarehe 18 Oktoba, 2021 na Kumb.Na. FA.170/371/O1"A"/111 cha tarehe 20 Septemba, 2021 vyote kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mchanganuo wa nafasi hizo ni kama ufuatao: -

1. MTENDAJI WA KIJIJI DARAJA LA III - *Nafasi 2*

(a) KAZI NA MAJUKUMU

- i. Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji.
- ii. Kusimamia Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao kwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji.
- iii. Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji.
- iv. Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji
- v. Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu.
- vi. Kuandaa taarifa ya utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha Wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali.
- vii. Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vyatia Kitaalam katika Kijiji
- viii. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na Nyaraka za Kijiji.
- ix. Mwenyekiti wa Vikao vyatia Wataalamu katika ngazi ya Kijiji.
- x. Kupokea na kutatua matatizo / malalamiko ya wananchi

- xi. Kusimamia utungaji wa Sheria ndogo za Kijiji na
- xii. Kuwajibika kwa Mtendaji wa Kata.

(b) SIFA ZA MWOMBAJI

- i. Awe na Cheti cha Kidato cha Nne (IV) / Sita (VI)
- ii. Awe amehitimu mafunzo ya Astashahada / Cheti ambayo ni NTA (Level 5) katika moja ya fani zifuatazo: - Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambulika na Serikali.

(c) Ngazi ya Mshahara

TGS. B1 : 390,000/= kwa mwezi

2. MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU II - *Nafasi 1*

(a) KAZI NA MAJUKUMU

- i. Kutafuta kumbukumbu / nyaraka / mafaili yanayohitajiwa na wasomaji
- ii. Kudhibiti upokeaji, uandikishaji wa kumbukumbu / nyaraka
- iii. Kuchambua, kuorodhesha na kupanga kumbukumbu / nyaraka katika makundi kulingana na somo husika (classification and boxing) kwa ajili ya matumizi ya Ofisi.
- iv. Kuweka / kupanga kumbukumbu / nyaraka katika reki (file racks / cabinets) katika masjala / vyumba vya kuhufadhia kumbukumbu.
- v. Kuweka kumbukumbu (barua, nyaraka nk.) katika mafaili.
- vi. Kushughulikia maombi ya kumbukumbu / nyaraka kutoka Taasisi za Serikali.

(b) SIFA ZA MWOMBAJI

- i. Awe na Cheti cha kuhitimu Kidato cha Nne (IV) / Sita (VI)
- ii. Awe na Cheti cha Utunzaji kumbukumbu katika mojawapo ya fani za Afya, Masjala, mahakama na Ardhi.

(c) Ngazi ya Mshahara

TGS. B1 : 390,000/= kwa mwezi

MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBALI WOTE AMBAO
NI LAZIMA KUZINGATIA

- (a) Mwombaji ni lazima awe raia wa Tanzania
- (b) Awe hajawahi kufungwa kwa makosa ya Jinai
- (c) Awe hajawahi kufukuzwa au kupunguzwa kazi Serikalini
- (d) Maombi ni lazima yaambatanishwe na vivuli vyta vya kuzaliwa, kuhitimu Elimu ya Sekondari (*Result Slips hazitakubaliwa*) na vyuo vya mafunzo au Taaluma.
- (e) Maombi ni lazima yaambatanishwe na picha mbili za "passport size" za hivi karibuni
- (f) Maombi ni lazima yaambatishwe na wasifu "Curriculum Vitae" zenyenye mawasilisno ya uhakika, Anuani, barua pepe na namba za simu.
- (g) Awe na Umri wa miaka 18 na usiozidi miaka 45
- (h) Mwombaji awe hajawahi kuajiriwa Serikalini na kupata cheki namba.
- (i) Waombaji wenyenye vyeti vya kidato cha nne na cheti cha taaluma ambavyo vimepatikana nje ya nchi wahakikishe vimehakikiwa na Baraza la Taifa la Mitihani (NECTA) na Baraza la Elimu ya Ufundji wa Taifa (NACTE)

Waombaji wote wenyenye sifa watume maombi yao kwenye anwani ifuatazo: -

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Meru,
S. L. P 462,
USA - RIVER.

Barua za maombi zinapokelewa kuanzia tarehe 07.01.2022 hadi tarehe 20.01.2022 saa 9.30 Alasiri.

Tangazo hili pia linapatikana kwenye Tovuti ya Halmashauri ya www.merudc.go.tz na mbao za matangazo katika Ofisi ya Makao Makuu ya Halmashauri na Ofisi za Vijiji na Kata zilizopo Halmashauri ya Meru.

Tangazo hili limetolewa na:

Zainabu J. Makwinya

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA MERU

MKURUGEZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA MERU
S.L.P. 462 USA RIVER
MERU - ARUSHA